TANGAZO LA SERIKALI Na. 242 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA UTAMADUNI NA VIBALI VYA BURUDANI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 816 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Utamaduni na Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Utamaduni na Vibali vya Burudani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

**2**. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 4 kwa kufuta maneno "harusi na" mara baada ya neno "tambiko" katika kanuni ndogo ya (4).

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

**3**. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza kwa kufuta maneno "na kadhalika" popote yanapojitokeza katika kipengele (d).

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi- OR-TAMISEMI*